Mambo Ya Kitoto

na

Ellis P. Forsman

Mambo Ya Kitoto

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Mambo Ya Kitoto

1 Kor. 13:11

1 Kor. 13:11, "*Nilipokuwa mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto.*"

Hiki ndicho kifungu tunachoona Mtume Paulo akielezea mambo ambayo yanapaswa kuwekwa pembeni mtu anapokuwa mtu mzima.

Anamuongelea mtoto kama mtu ambaye anapata taarifa nusu na mtu ambaye hana msingi; mtu ambaye uelewa wake ni mdogo na haujakamilika; mtu ambaye hana mtazamo wa vitu uliokamilika, na anayefahamu machache.

- Mtoto anaweza kuwekwa katika miguu ya furaha au ya huzuni kwa nyakati fulani, bali kujizuia mwenyewe kunatokea kwa kukomaa.
- Mtoto anaweza kufikiri, akabishana, na kufikiria katika hali ya udhaifu na tabia ya hitimisho.
- Mtoto anaukomo wa kukua katika maneno. 2 Pet. 3:18, "*Lakini kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"
- Mtoto hana ujuzi kamili wa neno la Mungu.
- Mtoto hatumii kauli ya mtu aliyekomaa.

Kuna baadhi ya chembe chembe za kitoto ambayo tunahitaji tusiyaweke pembeni

Watoto hawana lawama, warahisi, wasafi, na hawana lawama.

- Mt. 19:14, "*Lakini Yesu akasema, waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie kwa maana walio mfano wa hao ufalme wa mbinguni ni wao.*"
- Mt. 5:8, "*Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu.*"
- 1 Tim. 5:22, "*Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine. Ujilinde nafsi yako uwe safi.*"

- 1 Pet. 1:22, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.*"

Watoto wanahamu ya ujuzi.

- 1 Pet. 2:2, "*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.*"
- Mt. 5:6, "*Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.*"
- Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Watoto wana moyo wa kusamehe.

Luka 23:34, "*Yesu akasema Baba uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake wakipiga kura.*"

Efe. 4:32, "*Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Kol. 3:13, "*Mkichukuliana na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo hivyo na ninyi.*"

Watoto wako tayari kuwa na upendo, wakarimu na kweli.

Watoto wanapenda kuvutana sana, hataivyo wanapenda kupigana.

- Mt. 22:37, "*Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka.*"
- Mt. 5:44, "*Lakini mimi nawaambia wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi.*"
- Mt. 19:19, "*Waheshimu baba yako na mama yako, na mpende jirani yako kama nafsi yako.*"

Watoto wanaimani ya kutegemea.

Wakiwa katika umri mdogo watoto uwa wanafikiria wazazi wao kuwa ni wazuri sana na hawawezi kufanya kosa.

Ndiyo, wanapokuwa wanafikiria wazazi wao kuwa ni viziwi; hiyo ni hadi watakapokuwa watu wazima, alafu baadaye tena wanafikiri wazazi wao kuwa hawana kosa.

- Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"
- Mt. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"
- 2 Tim. 1:12, "*Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.*"

Kuna baadhi ya mambo ya kitoto ambayo tunapaswa kuyaweka mbali

Watoto maranyingi ni wabinafsi.

Watoto wadogo maranyingi hufikiria tu kuhusu wao wenyewe na matakwa yao wenyewe, na sio wengine. Yakobo 4:3, "*Hata mwaomba wala hampati, kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tama zenu.*"

Mfano wa ubinafsi ni mkulima tajiri. Luka 12:16-21, "*Akawaambia mithali akisema, shamba la mtu mmoja tajiri lilikuwa limezaa sana; akaanza kuwaza moyoni mwake, akisema, nifanyeje? Maana sina pa kuyaweka hakiba mavuno yangu. Akasema nitafanya hivi; nitazivunja ghala zangu, nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kisha nitajiambia ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi. Lakini Mungu akamwambia mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.*"

Watoto wanaweza kuwa wakorofi na watundu.

Wanapaswa kutulizwa na kuweza kupendezeshwa. Wanaweza wakawa wanatamani vitu vya wengine.

Mfano wa kaka mkubwa katika hadithi ya mwana mpotevu. Luka 15:28-29, "*Akakasirika akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake akasema, tazama mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwana mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu;*"

Wivu ni tabia za kitoto.

Ndugu zake Yusufu walikuwa wakimwonea wivu.

- 1 Kor. 13:4, "*Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni;*"
- Mith. 14:30, "*Moyo uliomzima ni uhai wa mwili; bali husuda ni ubovu wa mifupa.*"
- Gal. 5:26, "*Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.*"

Watoto ni wavivu, wanakuwa na hasira, na kusengenya.

Paulo na Petro wanaonya kuhusu kunung'unika na kusengenya.

- 1 Tim. 5:13, "*Tena pamoja na hayo hujifunza kuwa wavivu, wakizunguka zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena maneno yasiyowapasa.*"
- 1 Pet. 2:1, "*Basi wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote.*"
- 1 Pet. 4:15, "*Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine.*"

Watoto kila mara wanatamani midoli mipya.

Wanatafuta kuwa na muda mwafaka. 1 Yoh. 2:15, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake.*"

Hitimisho

Tunahitaji maisha yetu yaendelee kukua hadi tukue katika neno la Mungu.

Tunapaswa kufikiria mambo ya kiroho na sio mambo ya kimwili.

Wakati washirika wa mwili wa Kristo wanapoweka mambo ya kitoto, watakuwa wanakaribia ukamilifu.